

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

01 - Utangulizi

AlhamduliLlaah - Sifa njema zote Anastahiki Allaah (سبحانه وتعالى) Pekee, Mola wa walimwengu, Rahmah na amani zimshukie Nabiy wetu Muhammad (صلى الله عليه وآله وسلم) na jamaa zake, na Swahaba zake (رضي الله عنهم) na wote waliotangulia kwa wema mpaka Siku ya Mwisho.

Muislamu mwenye uwezo, inamuwajibikia kwake kutekeleza nguzo ya Hajj mara moja katika maisha yake, isipokuwa akiwa na wasaa wa mali na afya na akipenda anaweza kuirudia tena. Hikmah ya kuwajibika mara moja katika maisha ya Muislamu ni kwa sababu ya taabu, mashaka na gharama zake ambazo ingelikuwa taklifu kwa Waislamu pindi ingeliwajibika zaidi ya mara moja. Hivyo basi, kuna umuhimu mkubwa wa Muislamu kudhamiria kuitekeleza ‘ibaadah hii tukufu bila ya mapungufu ili aikamilishe kisawasawa khasa kama inavyotakikana kwa taratibu zake na nidhamu zake kama ilivyopokelewa kutoka kwa Nabiy wetu (صلى الله عليه وآله وسلم). Aghlabu humsikia mtu kusema: “Natamani kwenda tena Hajj kwani sikufanya kadhaa na kadhaa,” au “Nimekosea kufanya kadhaa na kadhaa.” Hakuna shaka kwamba hata ukipata maelezo na mwongozo wa kutosha kabla ya safari huenda ukakosea bado, lakini angalau utakuwa na ujuzi fulani wa kukuongoza katika mengi kutokana na mafunzo utakayoyapata humu In Shaa Allaah. Anasema Allaah (سبحانه وتعالى)

﴿ هَلْ يَسْتَوِي الَّذِينَ يَعْمَلُونَ وَالَّذِينَ لَا يَعْلَمُونَ إِنَّمَا يَتَذَكَّرُ أُولُوا الْأَلْبَابِ ﴾

((Je, wanalingana sawa wale wanaouja na wale wasiojua?" Hakika wenyé akili ndio wanaokumbuka))¹

Kuitekeleza ukiwa na elimu na ujuzi nayo, itakupatia pia Radhi za Allaah (سبحانه وتعالى), na hilo halipatikani ila tu kwa kuitekeleza kutokana na mafunzo

¹ Az-Zumar (39: 9).

sahihi kabisa tuliyoyapata kutoka kwa Rasuli (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) ambaye alikuwa akisema alipoanza kuitekeleza:

((تَأْخُذُوا عَنِ الْمَنَاسِكُ))

((Mchukue kutoka kwangu Manaasik (taratibu) zenu))²

Tumejaribu kadiri tuwezavyo kukusanya mafunzo yatakayomwezesha Muislamu kuitekeleza ‘ibaadah hii kwa njia sahihi na sahali In Shaa Allaah, na hilo litapatikana pindi tu ukijiandaa vizuri kwa mafunzo yake. Kubwa zaidi kwa mwenye kunuia kufanya ‘ibaadah hii, ni kumwomba Allaah (سبحانه وتعالى) Amruzuku subira ya kila wakati na katika kila hali kwani hilo ndilo atakalohitaji zaidi huko.

Tumetegemea zaidi mafunzo mbalimbali ya Wanachuoni, kadhaalika kutoka katika kazi mbalimbali tulizokwishaandaa katika mtandao wetu www.alhidaaya.com.

Tutashukuru endapo tutatanabahishwa kwa kasoro au kosa lolote litakalokuwepo katika kazi hii ili tuweze kurekebisha na kuboresha zaidi mbeleni In Shaa Allaah.

22 Swafar 1434H – 5 Januari 2013M

Kimehaririwa 3 Dhul-Qa'dah 1436H

² Muslim, Abu Daawuwd, An-Nasaaiy na wengineo.